

MWENENDO WA KUFUATA

Kwa kuhimiza mapokeo ya kijamii ya vijana wanawake waliokuwa katika makundi yenyi kumiliki silaha mu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo

Dibaji imeandikwa na bi
Jeanine Mabunda Lioko

CHILD SOLDIERS INTERNATIONAL

Utungo wa kwanza (2017) (1ère édition)
Lugha ya asili : Kifransa

Umeandikwa na kutolewa na Child Soldiers International
9 Marshalsea Road
SE1 1EP London
Uingereza
Tél: +44 (0) 20 7367 4110
Fax: +44 (0) 20 7367 4129
www.child-soldiers.org

Picha za Mungulirwa Rodiguez
Wazo la Michael Windsor-Ungureanu
Imechapwa katika nchi ya Uingereza na Bowmans

Yaliyomo

p.2 **Shukrani**

p.5 **Dibaji**

p.7 **Utangulizi**
- Mazingira
- Ukomo

p.11 **A. Mateso makali : kukataliwa na jamaa na marafiki**
- Namna gani kuachiliwa na jamii kunawasumbua vijana wanawake
- Kuamsha mapokeo ya jamii

p.25 **B. Namna gani kijana mwanamke anaweza kurudisha tena samani yake aliyoipoteza ?**
- Kushiriki maisha ya jamii
- Maadibisho
- Majifunzo ya kiufundi na kazi zenyi kuleta pato
- Mlimo na Ufugo

p.43 **C. Msaada wa kisaikolojia na kijamii : mafaa ya kumsaidia mtu kwa kumsikiliza**

p.49 **D. Wa RECOPE : wa kwanza katika kazi ya kurudisha vijana wanawake waliotoka katika makundi yenyi kumiliki silaha katika maisha ya jamii**

p.53 **E. Vijana wanawake wanaoachiliwa : tufanyaje kwa kuwakomboa katika makundi yanayomiliki silaha?**

p.57 **F. Kuwakinga vijana wanawake wasiorozeshwe katika makundi Yanayomiliki silaha, wala wasirudishwemo**

p.66 **Mkaguo**

p.70 **Vifaa kwa utongo**

Remerciements

Child Soldiers International inataka kuwashukuru kwanza vijana wanawake waliotoka katika makundi yanayomiliki silaha waliokubali kutuletea ushuhuda wao. Na ni ushuhuda huo uliotusaidia kutunga kitabu hiki. Tunayo matumaini kama fikara tunayotolea katika kitabu hiki, itasaidia kuboresha maisha yao ya kila siku na maisha ya vijana wanawake wote wanaosumbuliwa na mizozo mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Shukrani zetu ziwafikie pia wale wote wanaousika na kuwakinga watoto (katika serkali ya Congo, mashirika zisizo za kiserkali na pia zile za kimataifa zenyi kutumika inchini Congo) waliotutolea muda na ujuzi wao kwa kutunga kitabu hiki. Kama vile :

- Ofisi ya mjumbe binafsi wa raisi anayeusika na kupiganisha ubakaji na kuingizwa kwa guvu kwa watoto katika makundi yanayomiliki silaha (BRP) ;
- Kamati ya kutimiliza mpango wa kupokonya silaha, kutoka katika kundi lenyi kumiliki silaha na kurudia katika maisha ya jamii (UEPN-DDR) ;
- Tawi la serkali lenyi kuusika na mambo ya kijamii (DIVAS) ;
- Mshauri wa Gavana wa jimbo la Kivu ya kaskazini anayeusika na mambo ya jamii, jamaa, wanawake na watoto;
- AGAPE/Hauts-Plateaux ;
- Muungano wa vijana kwa ajili ya maendeleo ya jamii – Lubarika (AJDC) ;
- Muungano wa vijana kwa ajili ya maendeleo kamili – Kalundu (AJEDI-Ka) ;
- Muungano wa watu wa mapenzi mema kwa ajili ya watoto yatima, walioachwa na wazazi wao, wasiopa-ta malisho bora na waliohamishwa kwa ajili ya vita (AVREO) ;
- Ofisi ya wenyi kujitoa kwa ajili ya watoto na kwa ajili ya afya (BVES);
- Shirika CARITAS ya jimbo ya Goma;
- Umoja wa makundi yasiyokuwa ya serkali ya humu nchini kwa ajili ya maendeleo ya msinji (COLDEBA) ;
- Kamati ya jimbo la uhaki na amani (CDJP) ;

- Shirika la wenyi kuusika na vijana na watoto wenyi kuachiliwa (CAJED);
- Muungano kwa ajili ya uvumilivu (Coopérative de la patience/ COOPA);
- Shrika la Don Bosco ;
- Mpango wa kupiganisha umaskini na taabu (PAMI) ;
- RET International ;
- Muungano wa walimaji kwa ajili ya maendeleo kamili katika vijiji (UPADERI) ;
- Muungano kwa ajili ya kutetea haki za watoto katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (UPDECO) ;
- Shirika Save the Children katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ;
- Shirika War Child UK katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ;
- Tawi la Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Watoto katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (UNICEF) ;
- Utume wa Umoja wa mataifa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (MONUSCO) ;
- Kamati ya kimataifa ya Msalaba mwekundu katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (CICR).

Kwa mwisho, tunamshukuru kwa namna ya pekee, Marie de la Soudière, mwandishi mkuu wa kitabu hiki na mtaalamu wa akili timamu na wa msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa watoto wenyi kusumbuliwa na mizo-zo ya wanaomiliki silaha. Shukrani pia kwa Boniface MUSH'AYUMA kwa msaada wake na mashauri yake wa-kati wa utungaji wa kitabu hiki

Dibaji

Myaka hii iliyopita, kumeonekana maendeleo ya kweli kwa kukomesha hali ya kuwatumia watoto katika makundi yenyi kumiliki silaha katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Mwaka wa 2012, kumekubaliwa mpango wa kupiganisha kuorozeshwa na kutumiya watoto katika makundi yanayomiliki silaha, na mpango wa kupiganisha hali ya askari jeshi na ya wanaousika na usalama wa nchi, ya kutoheshimu haki za watoto. Mpango huo umesaidia kutiwa kwa matengeneo na kutiwa kwa njia mbalimbali za kukinga watoto na za uwajibikaji, vilivyoleta maendeleo hayo.

Miongoni ya matengeneo hayo, Ofisi ya mjumbe binafsi wa raisi anayeusika na kupiganisha ubakaji na kuingizwa kwa guvu kwa watoto katika makundi yanayomiliki silaha (BRP), iliyoundwa mwaka wa 2014, ime-kusudia hasa kushurulikia kukinga watoto wasiorozeshwe katika makundi yanayomiliki silaha na kupiganisha kutoazibiwa kwa wote wanaousika na mambo hayo. Vilevile ofisi ya BRP ilitumika kwa kuwarudisha katika jamii na kuwasaidia kiuchumi watoto wanaotoka katika makundi yanayomiliki silaha pale Kibumba, Rutshuru, Bunia na Aru.

Kufuatana na juhudi hiyo, jeshi la Congo haliwapokei tena watoto wadogo, lakini wengi wao wangali bado katika makundi yanayomiliki silaha katika inchi ya Congo. Myaka kumi iliyopita, zaidi ya watoto elfu arubaini na sita (46.000), wamekwisha ondoshwa katika makundi yenyi kumiliki silaha. Wengi wao ni wanaume. Vija-na wanawake wengi wangali bado katika makundi hayo na hawapokei msaada wa mpango wa kurudishwa katika jamii.

Kwa kusahihisha jambo hilo, na katika mawazo ya kutumika pamoja, BRP imekusudia kusindikiza Child Sol-diers International na washirika wake katika nchi, katika kutunga kitabu hiki chenyi ukomo wa kuraisisha kutoka kwa vijana wanawake katika makundi yenyi kumiliki silaha, kuboresha msaada kwa kurudia kwao katika maisha ya jamii na kuendelesha kurudi kwao katika maisha ya uraia. Kwa hiyo, tunafurahi kuunga mkono kitabu hiki chenyi kuleta mawazo yenyi kutoka katika jamii ili kuboresha mambo madogo madogo. Mawazo hayo, yanawasaidia wote wanaousika na kumkinga mtoto, na wasio na vifaa vya kutosha.

BRP itaendelea kuunga mkono ili kutimiliza mawazo ya kitabu hiki. Mahitaji yenyi Child Soldiers International aliyoyakuta kwa vijana wanawake si jambo lingine, ila ni haki yao kama inavyopatikana katika vitabu vya she-ria. Mawazo ya kitabu hiki yatatekelezwa katika mipango yetu ijayo ya kupokonya silaha na kutoka katika makundi yenyi kumiliki silaha.

Kama mjumbe binafsi wa raisi anayeusika na kupiganisha ubakaji na kuingizwa kwa nguvu kwa watoto katika makundi yanayomiliki silaha, nawaalika wanaousika na kukinga mtoto katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, watumie mawazo ya kitabu hiki katika kazi yao kwa ajili ya vijana wanawake wenyi kuwa katika ma-kundi yanayomiliki silaha, na wajikaze kukitajirishe kwa mawazo yao mapya na kwa ujuzi wao.

Madame Jeanine Mabunda Lioko
Mjumbe Binafsi wa Raisi anayeusika na kupiganisha ubakaji na kuingizwa kwa nguvu kwa watoto katika makundi yanayomiliki silaha (BRP)

Utangulizi

Mazingira

Uchunguzi uliofanywa na Child Soldiers International, maagizo ya Kamati ya Haki za Mtoto kwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, na mashauri ya makundi yasiyokuwa ya serkali ya humu Congo, yamesaidia Child Soldiers International kutunga mradi ambao ukomo wake ni kufanya mkaguo wa mipango ya kupokonya silaha na kuishi vizuri katika jamii (DDR) kwa ajili ya vijana wanawake wa chini ya myaka 18 wenyi kuwa katika makundi yenyi kumiliki silaha mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Katika mradi huo, kundi moja la uchunguzi limepitisha juma sita katika majimbo ya Kivu ya Kusini, Kivu ya Kaskazini na Uele ya Juu mwanzo wa mwaka wa 2016. Kundi hilo limezungumza na vijana wanawake 150 waliokuwa zamani katika makundi ya wanaomiliki silaha[1] , wanamemba 84 wa mtandao wa jamii kwa kukinga mtoto (Réseaux communautaires de protection de l'enfant: RECOPE), waalimu na waongozi wa masomo 12, waongozi wa makanisa 8, wanaousika na watumishi 46 wanaousika na mipango ya DDR na wajumbe 14 wa wakubwa wa miji. Ukomo wa mazungumzo hayo ulikuwa kujua namna gani vijana wanawake wanasaidiwa na mipango ya DDR, na kuangalia kama ma kazi hayo yote - hapo yanapofanyika - yanapatana, hasa zaidi kulingana na vijana wanawake wenyewe.

Majifunzo yaliyopita yameonyesha waziwazi[2] kama miongoni mwa watoto waliotoka katika makundi ya-nayomiliki silaha, hesabu ya vijana wanawake ni ndogo, hawapati msaada wa DDR sawa na vijana wanaume, na, ikiwa wameupata, haupatani na mahitaji yao ya kipekee. Kwa namna ya pekee, majifunzo yemeonyesha kwamba, ijapo matendo mbalimbali kwa ajili yao, vijana wanawake wanabaguliwa na kusemwa vibaya wanaporudi katika jamii.

Tena, mipango ya DDR haileti jibu la kutosha kwa magumu hayo wanaopata kwa kupokelewa katika jamaa na katika jamii.

Mwezi wa kumi, mwaka wa 2016, Child Soldiers International ameleta ripoti ya uchunguzi wake katika mku-tano wa pale Goma mbele ya wanamemba wa DDR, Ofisi mbalimbali ya Umoja wa mataifa, makundi ya-siyokuwa ya serkali (ONG) na wajumbe wa serkali. Waliohuzuria mkutano huo, wamesikiliza malalamiko na maagizo ya vijana wanawake yaliyoletwa na Child Soldiers International. Pia walifikiria kuhusu majibu kwa hayo yote kabla ya kukusudia nini itafinyika kwa ajili ya mahitaji ya vijana wanawake na kurahisisha, katika heshima ya haki zao, kwa kupokonya silaha na kwa kurudia katika maisha ya jamii

Ukomo

Kitabu hiki ni mchango wa mawazo yaliyoletwa katika mkutano wa Goma. Ni kama « sanduku ya vyombo » kwa kuwasaidia wanamemba wa DDR ili kuwashurulikia vijana wanawake waliokuwa katika makundi ya-nayomiliki silaha mashariki mwa Congo, katika mahitaji yao. « Sanduku ya vyombo » hii itawasaidia vilevile wanamemba hao kupiganisha na kushinda vikwazo ambavyo vijana wanawake wanavipata, ginsi walivyo-sema wao wenyewe[3], katika mpango wa kupokonya silaha na kurudia katika maisha ya kijamii. Mawazo mengi ya kitabu hiki si mapya. Makundi mengi yasiyokuwa ya serkali (ONG) yamekwisha kuyatumia mara nyingi. Lakini, mawazo hayo hayajulikani sana wala hayatumiwi vema na wanamemba wote wa DDR.

Wanamemba wenyi kuusika na kukinga mtoto ambao kundi la uchunguzi limekutana nao, wamesema kama hakuna tena pesa ya DDR kwa ajili ya watoto (tokea myaka miwili katika maeneo mamoja, na siku hizi katika maeneo mengine), ao pesa hizo ni kidogo mno zisiweze kusaidia, ila sehemu ndogo tu ya watoto miongoni mwa wale wenyi kuwa katika makundi yenyi kumiliki silaha.

Kwa sababu hiyo, isipokuwa kwa mpango wa masomo, kitabu hiki kinazungumzia kuhusu kazi isiyoomba pesa nyingi na inayoweza kutumiwa na wanamemba wenyewe wa jamii wakisaidiwa na vyote walivyo navyo katika jamii yao. Mara mojamoja, msaada wa mwanzo (wa kiufundi ao wa vitu) unaweza kuhitajika. Hapo, utatoka kwa kamati ya kutimiliza mpango wa kupokonya silaha, kutoka katika kundi lenyi kumiliki silaha na kurudia katika maisha ya jamii (UEPN-DDR), kwa Tawi la serkali lenyi kuusika na mwanamke, jamaa na mtoto (DIVIFFAE), kwa Tawi la serkali lenyi kuusika na mambo ya kijamii (DIVAS) ao kwa mfanya kazi wa DDR.

Maelezo machache ya lazima :

- **Kitabu hiki hakileti mawazo yote kuhusu mpango wa kupokonya silaha, kutoka katika kundi lenyi kumi-liki silaha na kurudia katika maisha ya jamii** (DDR) kwa ajili ya vijana wanawake mashariki mwa Congo, wala hakileti mawazo ya mpango huo nje ya eneo hilo. Kitabu hiki kinatoa maagizo mazuri tulioyapokea na yenyi kusaidia kuepuka magumu yanayo-patikana katika mpango wa DDR kwa vijana wanawake. Watakaotumia kitabu hiki, wanaalikwa kuga-wanya kati yao mawazo yao ili kukitajirisha.

- Kwa kuwa kitabu hiki hakileti mawazo yote, kinapashwa kutumiwa pamoja na **mipangilio ya sasa kuhusu DDR kwa watoto**, na kwa namna ya pekee *Mashurti kuhusu watoto waliotoka katika makundi ya-nayomiliki silaha* (yanayoitwa **Mashurti ya Paris**) ya mwezi wa pili 2007. Tujue kama kitabu hiki hakichu-kui nafasi ya Mipangilio hiyo.

▶ **Maagizo ya kitabu hiki yaweza kutumiwa pia kwa ajili ya vijana wanaume waliotoka katika makundi yanayomiliki silaha**, kwani wao vilevile wameteswa sana walipokuwa katika makundi hayo na waliporudi katika jamii. Lakini kwa mawazo ya wanamemba wa DDR kwa watoto, mahitaji ya vijana wanaume yanatimizwa vizuri zaidi katika miradi iliyoko sasa kuliko mahitaji ya pekee ya wanawake, kama vile vinyume vya ubakaji na ku-semwasemwa vibaya katika jamii. Huo ndio ukomo wa kitabu hiki.

Notes

1. Ni vikundi mbalimbali vya Mai-Mai, FDLR (Vikundi ya kidemokrasia ya kukomboa inchi Rwanda), M23 na Kundi la Upingaji la Bwana (Lord's Resistance ArmyLRA).

2. Utume wa Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Ustawi katika Congo (MONUSCO), *Les rescapées invisibles : les filles dans les groupes armés en République Démocratique du Congo : 2009 à 2015*, 2015 : https://childrenandarmedconflict.un.org/wp-content/uploads/2015/11/rapport-monusco-filles-dans-les-groupes-armes-rescapees-invisibles.pdf ; Coalition pour mettre fin à l'utilisation d'enfants soldats (jina la zamani la Child Soldiers International), *Report to the Committee on the Rights of the child in advance of the DRC initial report on the Optional Protocol to the Convention on the Rights of the Child on the involvement of children in armed conflict*, 2011 : https://www.child-soldiers.org/shop/drc-opac-shadow-report-to-the-committee-on-the-rights-of-the-child-1.

3. Katika uchunguzi wake, Child Soldiers International, alikutana tu na vijana wanawake waliotoka katika makundi yanayomiliki silaha. Tunaweza kusema lakini kama mawazo mengi yaliyo katika kitabu hiki, yanaweza pia kutumiwa katika mpango wa kuwarudisha katika maisha ya kijamii vijana wanawake waliokuwa zamani katika makundi yanayomiliki silaha. .

A.

Mateso Makali: Kukataliwa na jama ana marafiki

« Afazali kufa huku, kwani jamaa yangu itanikana »

Namna gani kuachiliwa na jamii kunawasumbua vijana wanawake

Mara nyingi vijana wanawake waliotoka katika makundi yenyi kumiliki silaha waliishi vinyume mbali mbali ya mwili na kimoyo sawa vile ujeuri na kushtushwa kila siku kufa, hali ngumu ya maisha kwa namana pekee na kuachiliwa. Wanahitaji usikilivu, kutendewa mema na kupendwa, kwa kuweza kupona na kuendelea vizuri katika maisha mpaka hapo watakuwa na myaka ya mtu mzima.

Pahali pa hiyo, wanaporudi, wanabaguliwa, wanaachiliwa, wanazaniwa vibaya na hata kuzarauliwa. Wanaumizwa sana, na hali hiyo ndio chanzo cha mateso yao ya kiroho. Kufuatana na namna wanavyotendewa wanaporudi, hali ya kila mmoja wao ni tofauti:

- **Hasira na uasi** : wamoja wana hasira kwa sababu ya kuchukiwa na jamii. Hawakubali matendo hayo ya jamii yaliyo kwao ukosefu wa haki kufuatana na mambo walioyaishi, na wanakamata msimamo wa kupingana, wakijitia hivi katika mwenendo yenyi jamii iliwastaki kuwa nayo. Hali hiyo ya hasira inatokana na namna mbaya ya kupokelewa na jamii. Bahati mbaya, hali hiyo ya vijana wanawake inazidisha tena chuki ya jamii kwa ajili yao na inasababisha tena zaidi kutengwa kwao.

- **Kujizania mkosefu na kujitenga mwenyewe na wengine** : wengine wanachukua ndani mwao mazarau ya jamii na wanateseka bila kusema neno. Kwa sababu hiyo, wanajitenga wenyewe na maisha ya jamii japo walipenda kuwamo. Kwa mfano, wanajizuia kuwa pamoja na vijana wanaume na wanaepuka kushiriki michezo mbalimbali. Wamoja wanazani wanaweza kupokelewa na jamii wakitumika sana mashambani, wengine wakivumilia mazarau toka kwa watu. Wengi wanafikiri kama hakuna kitu kingine cha kufanya, isipokuwa kuvumilia hali hiyo.
- **Kurudi porini** : wengine tena wanashindwa kuvumilia mazarau ya jamii, na hivyo, wanakusudia kurudi porini katika kundi walimokuwa. Wanaona basi bora kuishi maisha ya mateso porini kuliko kutupwa na jamaa, na jamii lao.
- **Kukimbia** : vijana wanawake wengine, japo wangetamani kuishi pamoja na jamaa zao, wanakusudia kwenda kukaa nafasi nyingine za mbali ambako watu hawajui maisha yao ya zamani na kusio hasara ya kuzarauliwa na kukanwa. Vijana wa namna hiyo, hawajulikani kwa wanamemba wa DDR na hawapokei hata msaada mmoja: wanaishi katika hali ya upungufu mkuu. Vijana wanawake wengine tuliokutana nao, walihakikisha kama wenzao waliokuwa nao porini, kwa sababu ya hali yao ya upungufu, wanatumiwa na wengine kwa kiholela kwa kujipatia feza na kujifurahisha kimwili.

Kuamsha mapokeo ya jamii

Majifunzo yanaonyesha kama mapokeo mazuri ya jamaa na ya jamii yanasaidia zaidi kwa maendeleo ya kijana mwanamke aliyerudi kutoka porini, kuliko kusemwasemwa[4]

4. Joanne N. Corbin, *Returning home : resettlement of formerly abducted children in Northem Uganda* » in Disasters (Vol-ume 32, Issue 2, pp. 316-335), 2008 : http://onlinelibrary .com.doi/10.1111/j.1467-7717.2008.01042. x/abstract ; SWAY – The Survey of War Affected Youth, *Making reintergration work for youth in northem Uganda*, 2007 : http://chrisblattman.com/documents/policy/sway/SWAY.ResearchBrief.Reintegration.pd; Theresa S. Betancourt, Jessica Agnew-Blais, Stephen E.Gilman, David R. Williams, B.Heidi Ellis, « Past horrors, present struggles : The role of stigma in the association between war experiences and psychlosocial adjustment among former child soldiers in Sierra Leone » in So-cial Science and Medecine (Volume 70, Issue 1, pp.17-26), 2010 : htt://www.nobl.nlm.nih.gov/pmc/articles/PMC3756934./

« Mapokeo mazuri ya jamii yanasaidia kwa kupunguza upweke na kuongeza hali ya kujitumainia mwenyewe na ya kutamani kuishi ndani ya jamii, ijapokuwa hasara ya ujeuri. »

Tutie kukubaliwa kati ka jamii kuwa kiini cha nguvu zetu za kuwarudisha vijana wanawake katika jamii.

NAMNA GANI ?

Hatua A1 : Kuwahimiza watu muhimu wanaosimamia jamii.

NANI ? Mikutano kwa kuhimiza inaweza kutayarishwa na wafanya kazi wa DDR, na wengine wanaousika na kukinga watoto, wanamemba wa DIVIFFAE ao wa DIVAS, waprezidenti wa RECOPE, waalimu ao mtu yeyote aliyejifunza mpango wa kurudisha watoto katika maisha ya kijamii.

KWA NANI ? Watu wanaopashwa kuhimizwa ni :

- Jamaa za watoto waliotoka zamani katika makundi yenyi kumiliki silaha na majirani wao wa karibu ;
- Masultani wa asili na viongozi wa makanisa ;
- Wanamemba wa Baraza (shauri za wazee) ;
- Wanamemba wa RECOPE ;
- Viongozi wa masomo, waalimu na wanafunzi ;
- Vikundi vya wanawake ;
- Vikundi vya vijana na vya watoto ;
- Mtu yeyote ao kundi lenyi uwezo juu ya jamii.

NA NANI ? Ni vema kuwashirikisha katika mikutano vijana wanawake ao wamama waliotoka zamani katika makundi yanayomiliki silaha wakitamani.

WAKATI GANI ? Kazi ya kuhimiza inapashwa kuanzishwa haraka sana, kabla ya kurudi kwao vijana katika jamii ili kuwa hakika kama watasikilizwa na kupokewa vizuri watakaporudi. Ikiwa kama vijana wanawake wamerudisha silaha wao wenyewe, kazi ya kuhimiza

inapashwa kusindikiza hatua ya kwanza ya vijana wanawake waliokuwa kwanza katika kundi linalomiliki silaha ya kujijulisha katika jamii (Angalia wazo A4).

MAHAURI YA MUHIMU KWA WAHIMIZAJI :

- Kuwapasha wausika :
  - Kuhusu mateso vijana wanawake waliyoyapata ;
  - Vinyume vya kisaikolojia na vya kijamii vya maisha ya kale na ya sasa;
  - Hawastahili hukumu kwa sababu si kosa lao.
- Kuwashurulikia vijana wanawake katika mahitaji yao ya pekee. Kwa mfano, wahimizaji wanaweza kuonyesha namna gani, muda wa maisha yao yote, vijana wanawake waliokuwa katika makundi ya kigeni na ya kabila lingine yanayomiliki silaha ao wale wanaorudi kutoka porini wakiisha kuzaa, wana-semwasemwa katika jamii.
- Kufasiria kama, mara nyingi, hali ya vijana wanawake hao, ni vinyume vya kutopokewa na jamaa, ao ni vinyume vya woga wa kukataliwa na jamaa ; kufasiria kama wanaweza kujitenga na wengine na japo wanatamani kuwa pamoja nao. Kujulisha kama ikiwa jamaa na jamii inawakubali na kuwasaidia vijana hao, hali yao itaboreka
- Kukazia madaraka ya jamaa na ya jamii ya kuwasaidia vijana wanawake wapate nafasi yao ndani ya jamii (kama watoto wote waliokuwa katika makundi yenyi kumiliki silaha). Kuwajulisha kama wa-naweza kufaidika na msaada ao na mashauri kama wanayahitaji (kwa njia ya kundi isiyokuwa ya ser-kali (ONG), wanamemba wa RECOPE ao wa DIVAS, ao ya kundi ya kijamii inayousika na mpango wa kurudisha watoto katika maisha ya kijamii (groupe communautaire de reintégration). (Angalia wazo A3)
- Kuwaomba wale wote wanaohimizwa waondoe mawazo yao mabaya na wasiwahukumu vijana wa-nawake wanaorudi kutoka porini.

! **Haifai kuzungumzia matukio na mateso ya binafsi**, lakini kuzungumza kwa jumla tukileta mifano wazi ya mateso walioyaishi vijana wanawake waliotoka kati-ka makundi yanayomiliki silaha ili kuamsha usikivu na huruma ya jamii kwa ajili ya kundi nzima ya wale vija-na wanawake.

Hatua A2 : Kuwaandalia sherehe ya mapokeo vijana wanawake wanaorudi.

SABABU GANI ? Ukomo wa ibada hiyo ni kuwatakia ujio mwema watoto wanaorudi nyumbani baada ya mateso mengi, na kuonyesha mapashwa ya jamaa na ya jamii ya kuwashurulikia na kuwatunza watoto wao.

NAMNA GANI ? Ibada hiyo yaweza kuwa ya aina mbalimbali: ibada ya asili, ao sala, ao karamu ya chakula, ao maneno ya shukrani kwa ujio wa kijana mwanamke.

NA NANI ? Ibadi hiyo itakuwa na maana zaidi kama inaongozwa na mzee mheshimiwa wa jamii, na kama watu wengi wa jamii wanaihuzuria.

WAKATI GANI ? Siyo nyuma bado! Ibada ya namna hiyo imeonyesha lazima yake hata kisha myezi, hata myaka, baada ya kurudi kwao vijana wanawake. Tujiulize basi kuhusu mafaa ya ibada hiyo kwa ajili ya vijana wanawake wanaondelea kutungwa muda mrefu baada ya kurudi kwao. Ni lazima sana, kwa afya yake ya kisaikolojia, mtoto akiweza kuishi vizuri mahali alipopokewa wakati wa kurudi kwake, kuliko vyote alivyoishi ndani ya kundi lenyi kumiliki silaha.

MASHAURI YA MUHIMA KWA WALE WANAOANDAA IBADA HIZO

- Kuwaomba wote wanaohuzuria ibada kumpokea vizuri kijana mwanamke anayehitaji mapendo yao na msaada wao ; wawe wavumilivu kwake kwa sababu aliteswa ya kutosha ; na kumsaidia kupata nafasi kati yao, hata kama ni jambo gumu.
- **Watoto wa vijana wanawake wenyi kurudi wanapashwa kupokelewa na kukubaliwa kama wanamemba kweli wa jamii.**
- Ikiwezekana, kula na kunywa pamoja wakati wa ibada.

! **Yafaa kuepuka kuwashurtisha vijana wanawake kujionyesha kwa watu kama wao wenyewe hawataki.** Ni vema kuzungumza nao ili kuwaonyesha mafaa ya ibada hiyo.

« Mapokeo mazuri ya jamii yanasaidia kwa kupunguza upweke na kuongeza hali ya kujitumainia mwenyewe na ya kutamani kuishi ndani ya jamii, ijapokuwa hasara ya ujeuri. »

Hatua A3 : Kuunda vikundi vya kijamii yenyi kuusika na kuwarudisha vijana wanawake katika maisha ya jamii.

SABABU GANI ? Ukomo wa vikundi hivyo ni kuisaidia jamii kuwapokea vijana wanawake na kuwaheshimisha. Kuna njia mbili ya kuufikia ukomo huo :

> **Kuhimiza** mara nyingi jamaa na jamii kuhusu mateso ya zamani na ya sasa ya vijana wanawake ili watu wapate kuwa na hali nzuri mbele yao ;
>
> **Kuwatayarishia** wanamemba fulani wa jamii majibu kwa magumu yatakayowafikia wale vijana wanawake.

NANI ? Katika vikundi hivyo, sherti muwe watu fulani wanaosimamia jamii (viongozi wa makanisa, wanamemba wa baraza, waalimu, waprezidenti wa RECOPE...), jamaa za vijana wanawake waliokuwa zamani katika makundi yanayomiliki silaha na za wale bado wangalimo, na vijana wanawake waliokwisha kurudishwa katika maisha ya jamii.

MASHAURI YA MUHIMU KWA WANAMEMBA WA VIKUNDI VYA JAMII VINAVYOUSIKA NA KURUDISHA VIJANA KATIKA MAISHA YA JAMII

- Wakutane mara nyingi kwa kukamata mipango ya kuendelesha kazi ya kuhimiza jamaa na jamii, kwa kufikiria kuhusu njia mbalimbali ya kuwarudisha vijana katika maisha ya jamii, pia kufanya mkaguo wa kazi inayofanyika ili kuitimiliza kabisa.

Kuhimiza

- Kufikiri, katika upekee na pamoja, kuhusu kuingizwa kwa vijana wanawake katika makundi ya-nayomiliki silaha.
- Kuchunguza pamoja ginsi hukumu wanao kwa ajili ya vijana wanawake hao haupatani na mateso yao. Kuwajulisha kama hukumu wao huo unaweza kuwa kikwazo kwa kurudia kwa vijana wanawake hao katika maisha ya jamii na pia kwa kuboresha mwendo wao.

Mapadri wazungumzie shida za vijana wanawake katika hotuba zao.



- Kutafuta katika jamii ni wanani wanastahili kuhimizwa zaidi, kwa upekee ao wote pamoja. Kwa mfano :

- Viongozi wa makanisa (Mapadri, Mapasta, na Waimamu) wanaweza, katika mahubiri yao, kuzun-gumzia mateso ya vijana wanawake hao na ukosefu wa haki unaofanyika kwa ajili yao, na hivyo kuamsha ndani ya waamini hali ya usikivu na uvumilivu na kujenga ndani mwao hamu ya kuwapokea vijana wanawake hao katika jamii.

- Waalimu pia wanaweza kuzungumza na wanafunzi wao, wakifiri mambo kama vile kutowasemasema vijana wanawake hao, uvumilivu, na kuchukua makusudio ya kutowasumbua kwa njia yoyote. Waalimu wajikaze kuwapa moyo vijana wanawake waliotoka katika makundi yanayomiliki silaha na watoto wengine wenyi kuachiliwa, wakiwatendea kwa heshima. Wanafunzi wanaweza vilevile ku-wazungumzia wazazi wao mambo hayo na kugeuka hivyo wajumbe wa vijana wanawake katika jamaa zao.

- Vikundi vyote vinaweza kuandaa mikutano ya mazungumzo katika jamii kwa kupiganisha tabia zi-nazowashutumu vijana waliokutana kimwili na wanaume nje ya ndoa.

- Kutembelea mara nyingi jamaa ambamo, vijana wanawake waliotoka katika makundi yanayomiliki silaha ao waliobakwa, wanazidi kushutumiwa, wala hawajapokelewa bado vizuri, ili kuwahimiza wazazi.

- Kukazia pia mapokeo ya watoto vilema ao wenyi upungufu fulani katika jamii.

Matendo ya kutimiza

- Kufikiri pamoja kuhusu matendo ya kutimiza ili kuendelesha mapokeo katika jamii na heshima ya jamii kwa vijana wanawake (Angalia nukta B : Namna gani kijana mwanamke anaweza kurudisha tena ubora wake aliyoupoteza ?)

Waalimu wazungumze na wanafunzi wao kuhusu mambo kama vile kuwavumilia wengine, kutowasemase-ma vijana wanawake waliorudi kutoka porini.

Hatua A4 : Kuwatafuta vijana wanawake walipokonya silaha wao wenyewe na ambao hawapati msaada wowote.

NA NANI ? Kazi hii ni ya UEPN-DDR, DIVIFFAE, DIVAS na RECOPE wakisaidiwa na vikundi vya kukinga watoto.

KWA AJILI YA NANI ? Vijana wanawake waliorudisha silaha wao wenyewe ao wale walioachwa na makundi yanayomiliki silaha ambao hawakupata msaada hata kidogo. Hata kama hakuna pesa, ao hazitoshi, vijana wanawake wote waliotoka katika makundi yanayomiliki silaha wanahitaji kusaidiwa na wanamemba wa DDR, kwa namna ya pekee wale bado hawajapokelewa katika jamaa ao jamii zao.

MASHURI YA MUHIMU KWA WANAMEMBA WA DDR

- Kuwauliza vijana wanawake wote waliokwishatoka katika makundi yanayomiliki silaha kama wana-wajua wengine waliokuwa pamoja nao porini na ambao hawajapokea msaada hata kidogo. Ikiweze-kana, wao wenyewe wawatafute na kujua kama wanakubali kusaidiwa.

- Kutia usiano na kijana mwanamke yeyote anayehitaji kusaidiwa na kujua mahitaji yake :
  - Amepokewa vizuri katika jamaa na jamii yake ao yafaa asaidiwe kwa kumpatanisha na jamaa ?
  - Anatengwa mbali na wengine na anahitaji msaada kwa kurudia katika maisha ya jamii ? (Angalia ma-wazo B1 na F4)
  - Kufanya uchunguzi mdogo kwa kujua anaishi namna gani, anafanya kazi gani, nani anashurulika naye... kwa kujua kama kuna watu wengine, wakiona upungufu wake, wanamtumia kwa kujipatia faida.
  - Kuna mtu wa lazima anayeweza kuzungumza naye ? (Angalia wazo C1)
  - Kama ametoka sasa hivi katika kundi linalomiliki silaha, ni lazima apelekwe katika kituo cha afya ili apimwe.

! **Kujua kulinda siri.** Tufanye angalisho ili njia tunazotumia kwa kuusiana na vijana wanawake hao isitoe siri ya maisha yao, isi-wazaraulishe na kuwaletea fezeha zaidi. Kwa mfano kuwaalika kwa kuzungumza nao hazarani.

Kuwatafuta vijana wanawake walipokonya silaha wao wenyewe na ambao hawapati msaasa wowote.

Mwalimu mmoja anaweza kuunda timu la kabumbu munamo vijana wanawake na watoto wengine wa jamii.



B.

Namna gani kijana mwanamke anaweza kurudisha tena samani yake aliyoipoteza » ?

« Kila siku majirani wanasema kama tumetembea kimwili na wanaume. Haturuhusiwi tena kuwatembela mabinti wao. »

Vijana wanawake wengi, wafanya kazi ya DDR na wanamemba wa RECOPE tuliongea nao wanashuhudia kama vijana wanawake wanaotoka porini « wamekwishapoteza samani wao » kwa sababu «wametembea kimwili na wanaume».

Tukubali kama jambo hilo kweli limetukia, lakini tujaribu pia kubadilisha hali hiyo: watu wengi tulioongea nao wanasema kama vijana wanawake, japo maisha yao ya zamani, wangepata hali mpya ya maisha na kazi bora, wangelikubaliwa kwepesi ndani ya jamii.

Tuwasaidie vijana wanawake kwa kutambua na kupata nafasi njema na inayokubaliwa ndani ya jamaa na jamii.

NAMNA GANI ?

Kusharikia maisha ya jamii

« Ni wao wenyewe* [vijana wanawake] *wasiopenda kushiriki katika makundi ya vijana. Wanaume wanawashota vidole na kusemasema juu yao. »
(Mwanamemba wa RECOPE)

Kwa kupata tena heshima na furaha ya kuishi ndani ya jamii, mtoto anapashwa kupata tena nafasi yake ndani ya jamaa na jamii, mahali ambapo ataishi maisha ya kawaida kama wengine. Kuna ushuhuda kweli humu Congo na mahali pengine kama kijana mwanamke akipewa kazi ya kutumika ao akialikwa kusharikiana na kundi fulani, hasa kama wazo hilo linatoka kwa mwenyi kuheshimika ndani ya jamii, hiyo itamrudishia heshima kubwa na samani yake kati ka jamii.

Hatua B1 : Kuwasharikisha vijana wanawake katika kazi zinazo andaliwa na jamii na kwa ajili ya jamii.

SABABU GANI ? Kazi hii haiombi pesa nyingi, lakini ni ya muhimu kabisa kwa maana inamsaidia kijana mwanamke kupata tena samani yake na pia inamsaidia kustahili polepole matumaini ya jamii yake. Jambo hilo liwe shuruli ya kwanza.

NINI ? Kazi hizo zinaweza kuwa kwa mafaa ya wote ao kwa kujifurahisha katika jamii. Kushiriki kazi hizo, kutampatia tena kijana mwanamke nafasi katika jamii.

NA NANI ? Waheshimiwa wa jamii wanaweza kuomba kazi hiyo ambamo vijana wanawake watashirikishwa. Tena, washurulike katika hiyo kazi yao kuwasaidia jamaa na jamii wawatumainie watoto wao waliorudi kutoka porini na kubadilisha mawazo yao juu ya watoto hao.

MASHAURI YA MUHIMU KWA WALE WANAOWASHARIKISHA VIJANA WANAWAKE KWA KAZI YA JAMII

- Kutafuta kazi (ya binafsi ao ya kundi) kwa mafaa ya mji ao ya tarafa na inayowawezesha watu wa jamii kutumainiana.
- Kuwaalika vijana wanawake washiriki furaha ao ibada ya jamii, ikiwa kwa watoto ao kwa wakubwa. Kama ibada hizo hazipo, ni vema kuzianzisha ili kuwasaidia vijana wanawake waliotoka porini wakutane na vijana wanawake wengine, hata vijana wanaume ikifaa. Kwa mfano :
    - Mwalimu angaliweza kuunda timu ya kabumbu munamo vijana wanawake na watoto wengine wa jamii, na kuchezesha matimu mara nyingi ;

- Mapadri na Mapasta (pasteurs) wanaombwa kuwasharikisha vijana wanawake ku matumishi ya paro-kia kama vile katika kundi la waimbaji ao katika kundi fulani la vijana katika shirika .

▶ Kuomba msaada kwa vijana wanawake waliotoka porini kwa kazi moja ya mafaa ya wote. Kwa mfano :

- Waongozi wa makanisa wangeweza kuomba msaada kwa vijana hao katika kazi zao ;
- Sultani wa muji anaweza kuwaomba vijana wanawake kupamba chumba kimoja kwa tukio fulani la jamii.

▶ Kuwa hakika kama kazi iliyofanywa na kijana mwanamke ipo wazi na inajulikana na wote, na apewe vifaa vyote kwa kuitimiza vema.

! **Si vema kumtenga kijana mwanamke anayekataa kusharikia kazi ya jamii.** Inawezekana kijana mwanamke asishiriki kazi hizo kwa sababu ya kuogopa masemi mbaya ya watu juu yake. Yafaa kuongea naye ili atambue kama anakaribishwa na kama hakuna neno baya litasemwa juu yake. Kuwa hakika kama jamii itampokelea vizuri na kumwalika kila mara.

Mapadri na viongozi wengine wa makanisa wajikaze kuwaingiza vijana wanawake katika makundi mbalimbali ya parokia kama vile waimbaji.



« Tangu nimerudi shuleni, watu wote wananifurahia na wananiomba shauri kunapokuwa shida. »

Maadibisho

« Ili wapate samani katika jamii, ni sherti wanawake wapelekwe masomoni . »
(Mwanamemba wa RECOPE)

« Tangu nimerudi shuleni, watu wote wananifurahia na wananiomba shauri kunapokuwa shida . Hali imebadilika kabisa kwani vijana wote wa jamii yetu wananiheshimu na kunialika katika mikutano ya vijana kwa kukamata mipango. »

Kufuatana na mawazo ya vijana wanawake wenyewe na ya RECOPE, masomo ni njia bora kwa kijana mwa-namke aliyetoka porini ya kupata tena samani yake na kupokelewa katika jamii. Masomo ni njia bora kwa kusahau hali yao ya kale, kwa kujihakikishia hali nzuri mpya na kwa kupata msamaha wa jamii.

Vijana wanawake wote tuliokutana nao wana tamaa kubwa sana ya kurudia shuleni, ao ya kujua tu kuandika na kusoma. Lakini, shida ni nyingi, kama vile ukosefu wa pesa na kusemwasemwa.

Hatua B2 : Kuwasaidia vijana wanawake wote waliotoka zamani katika makundi yanayomiliki silahaku-rudi shuleni ao kujufunza kusoma, kuandika na kuhesabu.

Masomo

NAMNA GANI ? Kwa kuwa, mara nyingi, pesa inakosekana kwa ajili ya masomo ya vijana wanawake, tunapashwa kutafuta njia ingine kwa kuwawezesha mtindo fulani wa masomo (Angalia mashauri hapa chini). Ni lazima nguvu zote kwa masomo zisindikizwe na kazi ya kuhimiza wazazi, waalimu na wanafunzi ili wapiganishe hali yao ya ubaguzi (Angalia Wazo A1).

Kujifunza kusoma, kuandika na kuhesabu (kisomo)

KWA NANI ? Vijana wanawake wote wasiojua kusoma, wanapashwa kujifunza kusoma, kuandika na kuhesabu, hata kama wanafuata mafunzo ya kiufundi ao hata kama wanapokea msaada kwa kazi inayowaletea pesa (Angalia wazo B3)

NA NANI ? Waalimu wanaojitolea kwa bure, wanamemba wa jamii wanaojua kufundisha (wanamemba wa RECOPE wanaousika na ukingo wa mtoto, waganga wanawake).

MASHAURI YA MUHIMU KWA WAZAZI, WAALIMU NA WANAOUSIKA NA KAZI YA UKINGO WA MTOTO

- Kuhimiza jamaa za vijana wanawake zinazowazuia watoto wao kurudi shuleni kwa sababu wametembea kimwili na wanaume. Kuwafasiria kama masomo ndio njia muhimu ambayo wanahitaji kwa kuweza kupokelewa katika jamaa.
- Kujikaza kukubaliana na shule fulani kwa kuwapokea kwa bure (ao wakilipa pesa ndogo) vijana wanawake waliotoka katika makundi yanayomiliki silaha. Masomo yanayopokea vijana wanawake hao, yanaweza kupata msaada kidogo wa pesa ao vitu (ukiwako).
- Kuzungumza na wafanya kazi wa DIVAS kwa kupata vyeti vyenyi kuonyesha hali yao, ili vijana hao wasome kwa bure, ao kwa pesa ndogo.
- Kujifunza pamoja na vijana wanawake na jamaa zao njia mbalimbali ya kuongeza pato lao kwa kulipa masomo. Mfano : kutafuta njia ya kuzidisha mavuno yao ya mashamba (Angalia mawazo B3 na B4).
- Kuwahimiza wafazili kwa ajili ya misaada yao ya kudumu kwa watoto waliotoka porini tukiwaonyesha mafaa ya masomo (Nukta C) na lazima ya masomo kwa kuepuka kuorozeshwa kwa watoto katika makundi yanayomiliki silaha, ao kurudi kwao katika makundi hayo.
- Kuandaa mafunzo ya pekee kwa kuwasaidia vijana wanawake wenyi umri wa kutosha, ili wafikie elimu ya wenzao wenyi umri wao. Mafunzo ya namna hiyo, ni rahisi.
- Kuandaa kisomo na majifunzo ya hesabu. Kisomo kinaelekea pia vijana wanawake wote wasioenda shuleni kwani hasara ni kubwa kwao ya kuorozeshwa katika makundi yanayomiliki silaha, na ya ku-bakwa. Vijana wanaweza pia kufundishwa kujua kuishi, usafi, haki za mtoto...
- Kujaribu kumpata mwalimu atakayejitolea kwa kazi hiyo kwa bure, ao kwa mshahara mdogo, kwa ajili ya kisomo na majifunzo ya hesabu, na kutumia vyumba vya masomo kwa bure.



Majifunzo ya kiufundi na kazi zenyi kuleta pato

« Sina haya ya kuuzisha makaa. Ndiyo yao inayoniheshimisha kwani nashiriki kwa maendeleo ya jamii yangu. »

Majifunzo ya kiufundi na kazi zenyi kuleta pato zinawafanya vijana wanawake kusaidia uchumi wa jamaa zao, wajitoshelee kiuchumi na watayarishe maisha yao ya kesho. Majifunzo ya kiufundi na kazi zenyi kuleta pato zinasaidia pia, na kwa sehemu kubwa, kuwarudishia samani vijana wanawake wanaotoka porini na kurahisisha mapokeo yao katika jamii.

Hatua B3: Kuwaletea vijana wanawake majifunzo ya kiufundi yenyi kuwastahili na kuwasaidia kuendelesha kazi bora zenyi kuleta pato.

KWA NANI ? Mafunzo na kazi hiyo, ni kwa ajili ya kila kijana mwanamke aliyetoka porini kadiri ya mahitaji yake na ya jamaa yake (Angalia mashauri hapa chini), pia kwa ajili ya vijana wa namna hiyo wenyi kuwa shuleni ao wenyi kufuata kisomo na hesabu. Kujifunza kazi yenyi kuleta pato, kunaweza kuongeza mapato kwa ajili ya majifunzo.

NA NANI ? Makundi yasiyokuwa ya serkali yana ujuzi zaidi kwa mambo ya namna hiyo, lakini yanaweza kusaidiwa na RECOPE na makundi ya kijamii ya kuwarudisha vijana katika jamii kwa kufuatilia kazi hizo. Ni vema vijana wanawake wenyewe washiriki mipango inayochukuliwa kwa ajili yao. Lakini, yafaa kufanya angalisho kwa maana hawana ujuzi wa kufaa kwa kutimiza mipango hiyo.

MASHARI UA MUHIMU KWA MAKUNDI YASIKUWAO YA SERKALI (ONG)

- Kuwa hakika kama mazao ya kazi yatanunuliwa kwepesi. Kujua vema mipaka : yafaa washonaji ao wasuka-nywele wangapi katika mji ? Wanapata kweli faida katika kazi yao? Kama sivyo, ni bure kuongeza kazi ya ushonaji katika mji huo.

- Ni vema wazazi wakubali majifunzo ya kiufundi na kazi zenyi kuleta pato na kujua kama mapashwa mengine ya pekee (masomo), ao ya jamaa (kushurulikia wandugu nyumbani, kazi za mashamba...) hayawezi kuwa vikwazo. Kujua pia ni msaada gani kijana mwanamke atapata nyumbani mwao.

- Kuwa hakika kama kuna pesa ya kutosha kwa kumaliza mafunzo na kwa kuwatolea vijana wanawake vyote wanavyohitaji kwa kazi yao. Kukamata mipango yote kwa kumsaidia kijana muda wa miezi sita baada ya mafunzo yake.

- Kutoa mafunzo kuhusu namna ya kuongoza viwanda vidogo na namna ya kufanya hesabu, hata kama ni kazi ndogo. Wengi wameshindwa kwa sababu ya kutojua kufanya hesabu vizuri.

- Kuandaa kisomo na majifunzo ya hesabu kwa vijana wanawake wasiojua kusoma ili waweze kufaidika vizuri na mafunzo kuhusu uongozi wa viwanda vidogo. Bila mafunzo hayo, kazi zote za kuleta pato zi-tashinda.

- Kuzungumza na jamaa juu ya utumivu wa mazao ya vyakula walivyovipewa tukikazia juu ya faida wata-kaoipata wote wakiyauzisha kuliko kuyala. Wakati wa shida kali, kutayarisha msaada wa zarura wa chakula kwa ajili ya jamaa ili kazi yenyi kuleta pato izidi kuendelea.

- Kuzungumza na wafanya kazi wa DIVAS kwa kupata vyeti vya hali yao ya umaskini mkuu, ili vijana wa-liotoka porini wasilipishwe kodi kwa kazi yao yenyi kuleta pato.

! **Umuhimu na mafanyikio ya kitega uchumi ni vya lazima sana**. Majifunzo ya kiufundi na kazi zenyi kuleta pato vitaboresha hali ya kuwa ya kijana mwanamke kama tu kijana huyo anafikia kupata mafanyikio. Kazi yoyote ianze na mkaguo wa kweli. Mara nyingi, kazi zenyi kuleta pato zisizojulikana katika jamii, hazileti mafanikio. Ni muhimu kabisa kufuatilia kazi.

Mlimo na ufugo

« Majirani wetu wana kondoo na mbuzi, tungetamani kupata pia. »

Vijana wengi tuliokutana nao jimboni mwa Kivu (Kusini na Kaskazini) na Uele wa Juu, wanaishi vijijini na, wote, wasomi na wasio wasomi, wanatumika ao katika mashamba ya wazazi wao, ao katika mashamba za wengine kwa kuishi. Jamaa zenyi uwezo, zilikuwa na ufugo wa wanyama.

Kuwatolea vijana wanawake waliotoka porini mafunzo kuhusu mlimo na ufugo, kutawaletea mapato ya kiu-chumi ya kudumu. Mafunzo hayo yatasaidia pia kuboresha mazao ya mashamba na ya ufugo kwa faida ya jamii nzima. Mafunzo ya namna hiyo, yana mafanikio zaidi kuliko yale ya kiufundi wanaotolewa watoto wa-liotoka katika makundi yanayomiliki silaha katika majimbo yenyi mizozo na ambamo mafanikio ya uchuuzi ni zaifu.

Ginsi tulivyosema hapa juu kuhusu mafunzo ya kiufundi na kazi zenyi kuleta pato, mafanikio ya mlimo na ufugo yanaweza kuwasaidia vijana wanawake kujitegemea kiuchumi, kutayarisha maisha yao ya kesho na kuwarudishia samani katika jamii.

Hatua B4 : Kuzidisha uwezo wa vijana wanawake katika za mlimo na ufugo.

KWA NANI ? Kwa ajili ya vijana wanawake wote wa vijijini wenyi ujuzi katika mlimo na ufugo.

NA NANI ? Makundi yasiyokuwa ya serkali yana ujuzi zaidi kwa mambo ya namna hiyo, lakini yanaweza kusaidiwa na RECOPE na makundi ya kijamii ya kuwarudisha vijana katika jamii kwa kufuatilia kazi hizo.

MASHAURI YA KWA MAKUNDI YASIOKUWA YA SERKALI (ONG)

- Kuchungua uwezo na mahitaji ya jamaa kuhusu mlimo na ufugo.
- Kutolea vyombo vya kazi vya mlimo, mbegu na wanyama kwa kuboresha na kuzidisha mazao ya ja-maa.
- Kuwaletea vijana wanawake mafunzo kuhusu ufugo, hata kama jamaa ina ufugo ili wawakinge wanyama na magonjwa na kuwaepusha katika hatari ya vifo.
- Kufuatilia kazi hiyo na kuleta msaada muda wa myezi sita na kuchunguza kama vyombo vya kazi vipo katika hali nzuri.

! Kuzidisha uwezo wa vijana wanawake katika mlimo na ufugo siyo kuwapatia tu vyombo vya kazi na wanyama wa kufuga. Kwa ajili ya mafanyikio zaidi na kwa kuboresha hali ya vijana wanawake katika ja-mii, ni vema kufuatilia kazi yao, kuwaletea mashauri, kuwapa moyo na kuwatolea msaada wa kiufundi..

« Ni lazima sana, kwa afya yake ya kisaikolojia, mtoto aweze kuishi vizuri mahali alipopokewa wakati wa kurudi kwake, kuliko vyote alivyoishi ndani ya kundi lenyi kumiliki silaha. »[1]

Notes

1. Ripoti ya uchunguzi wa Child Soldiers International : Vijana wanawake wanatamani : kuboreshwa kwa namna ya kutimiza kazi ya kuwaomba vijana wanawake kupokonya silaha, na ya kuwarudisha katika mai-sha ya jamii, 2017 : https://www.child-soldiers.org/shop/ce-que-disent-les-filles

« Nisingepata mashauri ya prezidenti wa RECOPE, ningerudi porini. »

C.

Msaada wa kisaikolojia na kijamii : Mafaa ya kumsaidia mtu kwa kumsikiliza

« Ni mara ya kwanza leo ninaulizwa ni nini iliotukia. »

Mpaka sasa, katika kitabu hiki, tumezungumzia kuhusu mifano ya msaada wa kisaikolojia kwani inasaidia sana katika mausiano ya kijamii na inaleta faraja kwa vijana wanawake waliotoka katika makundi yenyi kumiliki silaha.

Masomo, kwa mfano (Wazo B2), yana kazi muhimu kwa kumtengeneza kijana mwanamke katika hali yake ya kisaikolojia, kwani yanapunguza sana vinyume vya vita, kuondoa hali ya mvurugu wa akili unaoletwa na vita kwa watoto, na kumuongezea usabiti wakati wa shida. Kwa njia ya masomo, watoto walio katika taabu, wanapewa nguvu ya kuzishinda, wanajikubali ginsi walivyo na kupewa nafasi ya kujiingiza katika ushirika wa wenzao.

Kuna lakini njia ingine inayoweza kusahisha haraka misongo ya roho wanayo vijana wanawake waliopatwa na matukio mabaya zamani ao wanayoyapata sasa. Njia hiyo ni « Msaada kwa kusikiliza na wekevu ».

Zaidi ya robo tatu ya vijana wanawake tuliokutana nao, walionyesha wazi tamaa yao ya kupata mtu mmoja wanaomtumainia na ambaye wanaweza kujifungua kwake na kumfasiria shida wanazo sasa. Na wengine tena wangependa sana wapewe nafasi ya kufasiria magumu walioyapata katika maisha yao ya kale.

Kwa kweli, muda wa myaka nyingi, wamoja wao wametendewa kikatili mwilini na rohoni, na wengine wameten-da matendo yanayowasumbua hata sasa wakiyakumbuka. Hayo yote yanasumbua zamiri yao na kufanya vigumu maisha ya kila siku na hatua ya kurudi kwao katika maisha ya jamii, kwa matendo hayo waliishi haiwa-ruhusu kuwa na hali yenyi kupendeza jamaa na jamii zao.

Lakini, vijana wanawake tuliokutana nao, walikuwa na mawazo ya kama jamaa zao hazitambui wala kusikia shida zao. Wanajitambua kutengwa na kuachiliwa. Walikuwa na lazima sana ya kupokewa na kusikilizwa. Hiyo ingewasaidia kupunguza uzito wa mzigo wa zamiri yao. Vijana wanawake tuliokutana nao wametuuliza kama tutarudi tena kwao siku ingine kwa sababu walisikia wanatulizwa kabisa na ule muda mdogo tuliopitis-ha kwa kuwasikiliza na kusharikiana nao katika magumu yao. « Msaada kwa kusikiliza na wekevu » ni wa mu-himu kabisa.

« Nisingepata mashauri ya prezidenti wa RECOPE, ningerudi porini. »

Katika sehemu nyingine, wanamemba wa RECOPE wanatoa msaada mkubwa sana wa kisaikolojia, ulio kituli-zo bora kwa vijana wanawake wengi waliotoka porini na wenyi shida, na unaowasaidia kurudia katika maisha ya kijamii. Bahati mbaya, wanamemba hao wangali wachache mno, tena hawapewi vifaa wanavyohitaji kwa kazi yao (angalia kipindi D.).

Tuchukue muda wa kutosha kwa kuwasikiliza kwa wekevu vijana wanawake waliotoka katika makundi yanayomiliki silaha.

NAMNA GANI ?

Hatua C1 : Kuwatafuta na kuleta mafunzo kwa wanamemba wa jamii wanaotaka, na wanaoweza kuwasikiliza kwa wekevu na bila kuwahukumu vijana wanawake waliotoka katika makundi yenyi kumiliki silaha.

NA NANI ? Wanaoweza kufanya kazi hiyo ni wanamemba wa RECOPE, waalimu, viongozi wa makanisa, na pia mtu yeyote wa jamii ambaye kijana mwanamke mwenyi shida anaweza kumtumainia, mtu anayejua kujiweka mahali pa wengine na mwenyi kuyajua na kuyashurulikia mahitaji ya kijana mwanamke aliyetoka porini. Na kazi hiyo ifanyika muda wa myezi ya kutosha.

NAMNA GANI ? Kadiri ifaavyo, ONG, DIVIFFAE na DIVAS wawaletee mafunzo wasiri kwa kazi hiyo (angalia mashauri hapa chini). Kwa kawaida mafunzo hayo ni kwa siku chache tu. Isipowezekana, mwanamemba wa ukingo wa mtoto amfasirie msiri mawazo makubwamakubwa ya kazi hiyo ya msaada kwa usikivu na wekevu (angalia hapa chini), akikazia kwa namna ya pekee juu ya umuhimu wake na juu ya kulinda siri.

MASHAURI YA MUHIMU KWA WASIRI

- Kukutana mara nyingi na kijana mwanamke aliyetoka katika kundi lenyi kumiliki silaha, kumsikiliza na kuzungumza naye. Kushurulikia maisha yake na shida zake. Katika mazungumzo, kukazia zaidi juu ya yale yanayowezekana, kuwa na moyo na kumletea mashauri.

- Kutomhukumu kijana mwanamke aliyetoka katika kundi lenyi kumiliki silaha na kutohukumu matendo yake. Wasiri wanapashwa kumkubali kijana mwanamke aliyetoka katika kundi lenyi kumiliki silaha ginsi alivyo. Ndiyo shurti kwa kutimiza vema « Msaada katika usikivu na wekevu ».
- Kutomshurtisha kijana mwanamke aliyetoka katika kundi lenyi kumiliki silaha ajifasirie kuhusu tukio fu-lani la maisha yake ao atoe mawazo yake ya pekee.
- Kuwa hakika kama kazi hiyo yafanyika katika siri.
- Kumsaidia kijana mwanamke aliyetoka katika kundi lenyi kumiliki silaha apate msaada wa kijamii na wa afya anaouhitaji, hata kwa njia ya namba 117 (Angalia ukarasa wa mwisho)
- Kutomhaidia kijana mwanamke aliyetoka katika kundi lenyi kumiliki silaha jambo lolote lisilowezeka ao lililo gumu kwa kutimiza.

! **Kuwa tayari kwa kufuatilia kwa mfulilizo kazi hiyo muda wa kufaa.** Kama kuna kizuio, sherti kumtaya-risha na kumpasha kwa wakati. Kukatikiza kazi hiyo kwa rafla na bila kumjulisha kuna hasara kubwa kwa kijana mwanamke aliyetoka katika kundi lenyi kumiliki silaha kama vile kuondoa matumaini kwa msiri na kufungua tena vidonda vyake vya ndani.

Usabiti na uhodari wa watoto :
Kazi ya wenyi ujuzi katika ukingo wa mtoto kwa watoto waliotoka katika makundi yenyi kumiliki silaha katika nchi nyingi, imeonyesha kama watoto waliokuwa katika shida kubwa sana porini, wadumu kwa jinsi ajabu katika usabiti na uhodari. Watoto wengi, walipo pokewa na jamaa na jamii zao, wakipata majirani na wasiri wengine waliowasikiliza, waliweza kufanya kazi yenyi ilionekana kweli kuwa bora, na wakaendelea vema, bila shida nyingi, wakiishi maisha kama vile vijana wengine. Kama watoto wanaishi kweli katika hali hii, wachache tu ndio watahitaji msaada wa wataalamu kwa kuwafuatilia kisaikolojia.


PROTEGEONS
LES ENFANTS
PROTEGEONS
LES ENFANTS
PROTEGEONS
LES ENFANTS

D.

Warecope, ni wa kwanza katika kazi ya kurudisha vijana wanawake waliotoka katika makundi yenyi kumiliki silaha katika maisha ya jamii

« Namna gani tunaweza kuandika ripoti ? Hatuna kartasi . » **(Mwanamemba wa RECOPE)**

Ni wanamemba wa RECOPE wenyi kustahili kuendelesha na kusaidia kazi ya kuwarudisha kijana wanawake waliotoka katika makundi yenyi kumiliki silaha na wanaoweza kufanya usiano kwa ajili ya ukombozi wao kwa sababu walipewa utume wa kuwakinga wototo, na pia ni wanamemba wa kawaida wa jamii zinazowapokea watoto wanaotoka katika makundi yanayomiliki silaha. Wanapopata msaada wa makundi yasiyokuwa ya serkali (ONG), wanafanya kazi nzuri sana kwa ajili ya watoto waliotoka katika makundi yenyi silaha, wakiwatolea pia msaada wa usikivu na wekevu.

Lakini, tangu zamani sana, tunatarajia mafanikio kwa wanamemba wa RECOPE, japo hawana vifaa vya kutosha na si wengi. Wanamemba hasa wanawake ni wachache katika kundi hilo. Wengi kati yao hawana vifaa na mafunzo ya kutosha kwa kuwashurulikia watoto wenyi shida pamoja na vijana waliotoka katika makundi yenyi kumiliki silaha. Kazi ya watu hao wa mapenzi mema inapashwa kujulikana waziwazi. Ni lazima wajue kama wanakubaliwa na wanaweza kusaidiwa.

Tuwasaidie wa RECOPE walio wa kwanza katika kazi ya kuwarudisha vijana katika maisha ya jamii.

NAMNA GANI ?

Hatua D1 : Kukamata hatua muhimu ya kuleta mafunzo na msaada kwa ajili ya wanamemba wa RECOPE na kujulisha wazi wazi kazi yao.

NANI ? Kuwajua wa wanamemba wote wa RECOPE na wale wote wanaowasaidia (sous-RECOPE) katika vijiji. Ha-wa, mara nyingi, hawapati mafunzo na msaada, japo ni wao wanaofanya usiano kwa kuwakomboa watoto katika makundi yenyi kumiliki silaha.

NA NANI ? Kazi ya kuleta mafunzo kwa wanamemba wa RECOPE na wasaidizi wao ni mapashwa ya wote: DIVIFFAE, DIVAS, Umoja wa Mataifa na ONG.

MASHAURI YA MUHIMU KWA WALE WANAOLETA MAFUNZO NA MSAADA KWA AJILI WA RECOPE

- Kuhimiza zaidi wanamemba wa jamii kwa kujiunga na wa RECOPE na wa Sous-RECOPE. Wanawake pia wanaalikwa kuingia katika wa RECOPE, kwani wanawake wanaweza kuwasaidia vizuri zaidi vijana wanawake wanaotoka katika makundi yanayomiliki silaha.
- Kuwapa wa RECOPE na wa Sous-RECOPE vifaa ili wawasaidie jinsi inavyofaa wanawake waliotoka po-rini na waendelee kufanya usiano kwa kuwakomboa wale wangali bado katika makundi yanayomiliki silaha. Hii yamaanisha :
    - Kuandaa kila mara mafunzo, kufuatilia kazi, kuleta msaada na kutia moyo ;
    - Kusipokuwa mafunzo, kutolea vitabu vya mafunzo ;

- Kuwarahisisha usafiri, usiano kwa simu, kuleta vifaa vya ofisi (buku na kalamu) na nguo kwa kujikinga (mvua) ;

- Kuwa wajumbe wao mbele ya Serkali ya Congo (kwa ngazi zote) na mbele ya wafazili wengine ili kukusanya pesa kwa ajili ya mafunzo, na misaada kwa wa RECOPE na wa sous-RECOPE.


PROTEGEONS
LES ENFANTS
PROTEGE

E.

Vijana wanawake wanaoachiliwa : tufanyaje kwa kuwakomboa katika makundi yanayomiliki silaha ?

« Nawasihi, fanyeni nguvu ili kuwakomboa vijana wanawake walio bado katika makundi yanayo miliki silaha. Mara mojamoja, tunapata habari za kuleta hofu sana juu yao. »

Mausiano na makundi yenyi kumiliki silaha kwa ajili ya kuwaacha huru watoto yameendekezwa vema kabisa na MONUSCO, UEPN-DDR, ONG na pia wanamemba hodari wa jamii ; lakini mausiano hayo yamefanikiwa, hasa kwa vijana wanaume.

Inaonekana hivyo katika mizozo nyingi ambamo watoto wanaorozeshwa na kutumiwa na makundi yenyi silaha : hesabu ya vijana wanawake ni kubwa zaidi kuliko hivyo inaonekana, lakini kwa sababu mbalimbali tena zisizo kuwa nyepesi kuelewa, ni kugumu sana kwao kupokonya silaha kuliko kwa vijana wanaume.

Kwa kweli, inaonekana kama vijana wanawake wengi tuliozungumza nao, hawakurudisha silaha wao wenyewe, lakini wamekimbia na walisema ya kwamba waliwaacha huko nyuma yao « wa vijana wanawake wengi ». Tena, vijana wanawake wengi wanachagua kubaki na makundi yenyi kumiliki silaha kwa sababu wanaogopa haya na kuchekelewa wakirudi kwao.

Tujikaze kweli kwa kuwajua na kuwakomboa vijana wanawake toka makundi yenyi kumiliki silaha.

NAMNA GANI ?

Hatua E1 : Kuwapa moyo na kuleta mafunzo bora kwa jamii ili kuzungumza na makundi yeni kumiliki silaha kwa kutetea ukombozi wa watoto na wa vijana wanawake pia.

NANI ? Wenyi kustahili kufanya kazi hii ni wa sous-RECOPE na Baraza kwa sababu wanaishi katika vijiji ambamo munapatikana makundi yenyi kumiliki silaha. Ni hao wanaweza kufanya kazi ya mausiano kwa ukombozi wa vijana wanawake.

NA NANI ? Wale wanaousika na kazi ya kupokonya silaha (MONUSCO, UEPN-DDR, ONG) ndio wanapashwa kuleta mafunzo kwa wanamemba wa jamii na kuwapa moyo kwa ajili ya mazungumzo na makundi yenyi kumiliki silaha.

MASHAURI YA MUHIMU KWA WENYI KUUSIKA NA KAZI YA KURUDISHA SILAHA

- Kuleta mafunzo kwa wanamemba wa sous-RECOPE na Baraza, kuwarahisisha usafiri na usiano kwa simu ili kukutana na makundi yenyi silaha, kupata ukombozi wa vijana wanawake na kuwarudisha ndani ya jamii. Kuwaongoza kwa wenyi kuusika na misaada hiyo wanayohitaji (afya, DDR...)
- Kuwapelekea wa sous-RECOPE na Baraza vitabu vya majifunzo kama hakuna jinsi ya kufika vijijini wanamokaa.
- Kuwahimiza wanawake wengi wajitoe kwa kazi ya uhimizaji wa makundi yenyi kumiliki silaha ikiwa kama hiyo ni njia ya kuweza kukutana na vijana wanawake hao waliotekwa.

- Kutangaza habari ya kama kutumia watoto kama wafanya kazi ao kwa kutembea nao kimwili ni aibu na ukatili vyenyi kuapizwa na sheria. Kuleta mifano ya wakamanda wa makundi ya kikongomani ya-nayomiliki silaha waliohukumiwa kwa ajili ya kutumia watoto katika makundi ya silaha na kwa ajili ya ubakaji.

Hatua E2 : Hijapokuwa wavijana wanawake wangali bado porini, kuhimiza jamii na kuitambulisha mate-so wanao yaona huko na nahitaju yao ya kusikilizwa na ya kusaidiwa.

(Angalia Hatua A1)

NANI ? Kujua jamii zote ambamo watoto wameorozeshwa katika makundi yenyi kumiliki siliha, bila kungoja kuan-zishwa kwa kazi ya kupokonya silaha.

NA NANI ? Wafanya kazi wa DDR na wengine wote wenyi kuusika na kazi ya ukingo wa mtoto wenyi kuasiliana na jamii, ndio kweli wanaostahili kufanya kazi hiyo ; lakiniwanapashwa kutumika pamoja na wa RECOPE, Ba-raza na makundi mbali mbali yenyi kuusika na kazi ya kurudisha vijana katika maisha ya jamii, yakiwako.

KWA NINI ? Habari zinatawanyika haraka. Na vijana wanawake watakaosikia kama jamii zao ni tayari kwa kuwapokea, watafanya haraka kukimbia makundi zenyi kumiliki silaha, ikiwezekana, ao kwa kujijulisha kwenyi timu (kundi) la DDR.

MASHAURI YA MUHIMU KWA WAHIMIZAJI

- Kuendelesha kazi ya kuhimiza jamii kwa kuwakubali vijana wanawake walio bado katika makundi ye-nyi kumiliki silaha.
- Kutayarisha makundi ya jamii itakayousika na mapokeo katika jamii ili kuendelesha kazi ya kuhimiza wanamemba wote wa jamii kwa mapokeo ya vijana wanawake (angalia Hatua A3).
- Kutawanya habari juu ya jamii zilizohimizwa na zenyi kuwa tayari kwa kupokea vijana wanawake ili vijana wanawake wenyi kuwa bado katika makundi yenyi silaha wapate habari hiyo na iwasaidie kukamata hatua ya kurudia kwao, ikiwezekana.



F.

Kuwakinga vijana wanawake wasiorozeshwe katika majundi yanayomiliki silaha, wala wasirudishwemo

« Nawashauria vijana wanawake wengine wanaofikiri kama porini maisha ni mazuri, wabadilishe mawazo yao, kwani kule, hakika, kuna kifo. »

Majifunzo yetu yameonyesha wazi kama sababu za kuorozeshwa vijana wanawake katika makundi yenyi kumiliki silaha, ni nyingi na ya aina mbalimbali katika nchi yetu. Kwa jumla ya vijana wanawake tuliozungumza nao, wawili juu ya watatu (2/3) wamesema kama wamechukuliwa kwa nguvu na kundi lenyi kumiliki silaha; mmoja juu ya watatu (1/3) amesema kama ameingia katika kundi la wenye silaha kwa kutaka kwake mwenyewe.

Kwa mafasirio yao wenyewe, kuna sababu kubwa ine iliyowafanya wakusudie kujiunga na kundi yenyi kumi-liki silaha: kuacha masomo, lazima ya ukingo, nia ya kulipisha kisasi na umaskini. Lakini kuna pia sababu nyin-gine: shida mbalimbali katika jamaa na kuvutwa na marafiki.

Ilionekana pia, katika sehemu nyingine za kutosha, ya kama wammoja kati ya jamii (na kati yao wazazi, wa-sultani wa miji na hata wanamemba wa RECOPE) wanashirikina makundi ya kujikinga (self-defence) na inayomiliki silaha (Maï-maï) na wanashauria vijana kuingia katika vikundi hivyo.

Kwa kuzuia kuorozeshwa kwa vijana wanawake, ni lazima kujua sababu hizo zote na kuwajua wote, katika jamii, wanaoshiriki, kwa karibu ao kwa mbali, kazi ya kuoroza vijana wanawake.

Kuendelesha na kusaidia jamii katika kazi zao za kuzuia kuorozeshwa kwa watoto wao katika makundi yenyi kumiliki silaha

NAMNA GANI ?

Hatua F1 : Mbele ya yote, kuhimiza jamii katika kazi yao ya kuzuia kuorozeshwa kwa watoto.

NA NANI ? MONUSCO, UEPN-DDR, ONG na wafanya kazi wa DDR pamoja na DIVIFFAE na DIVAS ndio wana uwezo na maarifa ya kufanya kazi hiyo. Wanapashwa kwa vyovyote kuyasharikisha makundi yote yanayotumika kwa ajili ya jamii kama vile RECOPE (angalia Hatua 1)

MASHURI YA MUHIMU KWA WAFANYA KAZI WA DDR NA WAHIMIZAJI

- Kujua kwanza jamii zinazoshiriki na kuorozesha watoto.
- Kuandaa mara nyingi mazungumzo ya makundi katika jamii hizo pamoja na wasultani wa miji, vion-gozi wa makanisa, wanamemba wa RECOPE ili kuwajulisha kama ni aramu kuorozesha watoto hata kwa ajili ya kujikinga, kwa sababu hasara itakayotukia kwa watoto, na kwa namna ya pekee kwa vija-na wanawake, ni kubwa. Kwa hiyo, huweza kutumia kitabu cha kuhimiza cha **Child Soldiers International** chenyi kuandikwa katika Kifransa, Lingala na Kiswahili (ukiihitaji tuma simu kwa namba +243813182039 ao +243991102747).
- Kwa hiyo, kutumia njia ya kuhimiza « jirani kwa jirani » (mwenzi kwa mwenzi) - hata kwa watoto wa-liokuwa zamani katika makundi yanayomiliki silaha - wakichagua watoto waliokwisha kuhimizwa ma-somoni, kanisani ao mahali pengine katika jamii. Kuwajulisha kama kuoroza watoto ni aramu, kwani wanaweza kuwafikishia wazazi wao habari hiyo na hivyo kugeuka wajumbe wa kutetea katika jamaa na jamii zao

Hatua F2 : Kuwapasha wakamanda wa makundi yenyi kumiliki silaha ya kama kuoroza watoto ni aramu na kuwajulisha aina ya maapizo kwa kitendo hicho. (angalia Hatua E1).

NA NANI ? Kama ni makundi ya kujikinga (Maï-maï) ambamo wanamemba wao ni watoto wa jamii, ni masultani wa jamii ndio wanaweza na uwezo wa kuwahimiza wakamanda.

NAMNA GANI ? UEPN-DDR, MONUSCO, ONG, DIVIFFAE wanapashwa kwanza kujua vizuri nafasi yenyi kupatikana kila kundi lenyi kumiliki silaha na inayooroza watoto.

MASHURI YA MUHIMU KWA WAFANYA KAZI WA DDR NA WAHIMIZAJI

- Kuomba msaada wa watu na wa makundi (RECOPE, Sous-RECOPE, Baraza) waliokwisha fanya kazi ya namna hiyo na waliofanyikiwa kwa kukomboa watoto katika makundi yenye silaha.
- Kuasiliana na shirika « **L'appel de Genève** » ama « **Muito wa Geneva** » (+243 82 477 07 03), linachou-sika na mazungumzo na makundi yenye silaha kuhusu kuheshimu kanuni za kiutu, ili kupata msaada wa kiufundi.
- Kukiomba na kukitumia kitabu cha kuhimiza cha Child Soldiers International kilichotayarishwa kwa ajili ya mafunzo na ujumbe kuhusu kukomeshwa kwa kuoroza watoto katika makundi yenyi kumiliki silaha. Kitabu hicho kimeandikwa katika Kifransa, Lingala na Kiswahili.
- Kupasha habari kama kutumia watoto kama wafanya kazi ao kwa kutembea nao kimwili ni aibu na ukatili vyenyi kuapizwa na sheria. Kuleta mifano ya wakamanda wa makundi ya kikongomani ya-nayomiliki silaha waliohukumiwa kwa ajili ya kutumia watoto katika makundi ya silaha na kwa ajili ya ubakaji.
- Kuandikwe kitambulisho chenye kuhakikisha kukomeshwa kuorozeshwa na kutumia watoto kwa ajili ya vita na vijana wanawake kama wafanya kazi mabali mbali ao watumwa wa kimwili (« wake »).



Hatua F3 : Kuhimiza jamii na wafazili juu ya mafaa masomo katika kukinga watoto wasiorozeshwe.

KWA NINI ? Vijana wanawake wengi tuliokutana nao wameingia katika makundi yanayomiliki silaha kwa sababu wa-meacha masomo kwa ukosefu wa pesa ao kwa kuwa wazazi wao waliwatosha masomoni.

« Kutosoma kwa watoto kunasababisha kuorozeshwa kwao » (Membre d'un RECOPE)

« Babangu ameniachisha masomo. Nimekasirika sana na ndiyo maana nimeingia katika kundi la wa Maï-maï. »

NA NANI ? Wafanya kazi wa DDR pamoja na makundi ya ukingo wa mtoto katika jamii (RECOPE, Sous-RECOPE, ma-kundi ya kazi ya kurudisha katika jamii) ndio wanausika na kazi hiyo.

MASHAURI YA MUHIMU KWA WENYI KAZI YA KUHIMIZA

- Kuhimiza jamaa ya vijana wanawake wawatume watoto wao kwa masomo, wakiwajulisha ya kama masomo inawakinga watoto wasiorozeshwe.

- Kuwaonya wafazili wanaoleta pesa na misaada kwa kwa kazi za masomo na kwa ajili ya DDR ya kama masomo inawakinga vijana wanawake ; na kwa hiyo, kuomba pesa kwa ajili ya masomo na kisomo kwa vijana wanawake wengi zaidi (angalia Hatua B2).

Hatua F4 : Kuendesha mbele kuwasharikisha watoto katika Maisha ya jamii, hasa vijana wanawake wasioso-ma.

KWA NINI ? Wakubwa kama vile vijana wanawake wanakubaliana ya kama uvivu wa watoto wasiosoma unasababisha, kwa sehemu kubwa, kuingia kwao katika kundi yenyi kumiliki silaha. Zaidi ya masomo (angalia Hatua B2 na F3), yafaa kuwasukuma watoto washiriki kazi ya jamii inayoweza kuwajenga.

« Nimefukuzwa shuleni kwa sababu ya ukosefu wa pesa. Pahali pa kuwayawaya mjini, nimekusudia kwenda kuwasaidia porini. »

« Sisi wanawake wa porini, tunawayawaya huku na kule kwa sababu hatuna la kufanya, hakuna kazi. Ingekuwa vema tungeenda shuleni. Lakini sasa, bila masomo, tutafanya nini siku nzima ? »

NA NANI ? Wanamemba wa makundi ya kijamii (wanamemba wa RECOPE, makundi ya kijamii yenyi kuusika na kazi ya ku-rudisha katika maisha ya jamii), ndio wanapashwa kufanya kazi hiyo kwani wapo karibu na vijana wanawake na tena wanakaa katika jamii moja. DIVAS akipatikana mahali hapo, anapashwa pia kuwasaidia.

MASHAURI YA MUHIMU KWA WENYI KAZI YA KUHIMIZA

- Kuwasaidia vijana wanawake wasiosoma washiriki kazi ya kijamii wanayoiweza, na yenyi kuweza kuwapa mafunzo na kuwaheshimisha. Kwa mfano : kuwapa madaraka madogomadogo ndani ya makundi ya wa-kaaji na ma kundi la faida na mkopo na kuwasaidia wahuzurie mikutano.
- Kuwa hakika kama vijana wanawake wanahuzuria mara nyingi michezo. Kama hayapo, kukamata hatua ya kuianzisha. Kama kuna lazima ya vifaa fulani, inawezekana kuviomba kwa DIVAS, shirika la kiinchi (ONG lo-cale), UNICEF...
- Kuwaomba vijana wanawake waanzishe michezo kwa watoto wadogo zaidi na kuwasaidia wayaongoze vema.
- Kuwaomba waongozi wa masomo waruhusu vyumba vya masomo na viwanja vya michezo kwa ajili ya watoto wasiosoma ili wavitumie kiisha masomo.

Mkaguo

A. Mateso Makali : Kukataliwa na jama ana marafiki

Tutie kukubaliwa kati ka jamii kuwa kiini cha nguvu zetu za kuwarudisha vijana wanawake katika jamii.

A1: Kuwahimiza watu muhimu wanaosimamia jamii.

A2: Kuwaandalia sherehe ya mapokeo vijana wanawake wanaorudi.

A3: Kuunda vikundi vya kijamii yenyi kuusika na kuwarudisha vijana wanawake kati ka maisha ya jamii.

A4: Kuwatafuta vijana wanawake waliopokonya silaha wenyewe na ambao hawapati msaada wowote.

B. Namna gani kijana mwanamke anaweza kurudisha tena samani yake aliyoipoteza ?

Tuwasaidie vijana wanawake kwa kutambua na kupata nafasi njema na inayokubaliwa ndani ya jamaa na jamii.

B1: Kuwasharikisha vijana wanawake katika kazi zinazo andaliwa na jamii na kwa ajili ya jamii

B2: Kuwasaidia vijana wanawake wote waliotoka zamani katika makundi yanayomiliki silaha kurudi shuleni ao kujifunza kusoma, kuandika na kuhesabu.

B3: Kuwaletea vijana wanawake mafunzo ya kiufundi yenyi kuwastahili na kuwasaidia kuendelesha kazi bora zenyi kuleta pato.

B4: Kuzidisha uwezo wa vijana wanawake katika kazi za mlimo na ufugo.

C. Msaada wa kisaikolokia binafsi: mafaa ya usikilivu kwa wekevu

Tuchukue muda wa kutosha kwa kuwasikiliza kwa wekevu vijana wanawake waliotoka katika makundi yanayomiliki silaha.

C1 : Kuwatafuta na kuleta mafunzo kwa wanamemba wa jamii wanaotaka, na wanaoweza kuwasikiliza kwa wekevu na bila kuwahukumu vijana wanawake waliotoka katika makundi yenyi kumiliki silaha.

D. Warecope, wa kwanza katika hatua za kurudisha vijana wanawake katika maisha ya jamii

Tuwasaidie wa RECOPE walio wa kwanza katika hatua za kuwarudisha vijana katika maisha ya jamii.

D1 : Kukamata hatua muhimu ya kuleta mafunzo na msaada kwa ajili ya wanamemba wa recope na kujulisha wazi wazi kazi yao.

E. Vijana wanawake wanaoachilwa: tufanyaje kwa kuwakomboa katika makundi yanayomilii silaha ?

Tujikaze kweli kwa kuwajua na kuwakomboa vijana wanawake toka makundi yenyi kumiliki silaha.

E1 : Kuwapa moyo na kuleta mafunzo bora kwa jamii ili kuzungumza na makundi yenyi kumiliki silaha kwa kutetea ukombozi wa watoto na wa vijana wanawake pia.

E2 : Hijapokuwa wavijana wanawake wangali bado porini, kuhimiza jamii na kuitambulisha mateso wanao yaona huko na mahitaji yao ya kusikilizwa na ya kusaidiwa.

F. Kuwakinga huorozwa na kurudishwa katika makundi yanayomiliki silaha

Kuendelesha na kusaidia jamii katika kazi zao za kuzuia kuorozeshwakwa watoto wao katika makundi yenyi kumiliki silaha.

F1: Mbele ya yote, kuhimiza jamii katika kazi yao ya kuzuia kuorozeshwa kwa watoto.

F2: Kuwapasha Wakamanda wa makundi hayo yenyi kumiliki silaha ya kama kuoroza watoto ni aramu na kuwajulisha aina ya maapizo kwa kitendo hicho.

F3: Kuhimiza jamii na Wafazili juu ya mafaa ya masomo katika kukinga watoto wasiorozeshwe.

F4: Kuendesha mbele kuwasharikisha watoto katika maisha ya jamii, hasa vijana wanawake wasiosoma.

Le chemin de la réintégration est long et difficile, il commence quand la jeune fille quitte le groupe armé mais ne se termine que lorsqu'elle retrouve une place dans sa famille et sa communauté et ces derniers l'acceptent pleinement.

Vifaa kwa utungo

- **Ripoti ya uchunguzi wa Child Soldiers International : Vijana wanawake wanatamani :** kuboreshwa kwa namna ya kutimiza kazi ya kuwaomba vijana wanawake kupokonya silaha, na ya kuwarudis-ha katika maisha ya jamii, 2017 : https://www.child-soldiers.org/shop/ce-que-disent-les-filles
- **Kitabu cha uhimizaji cha Child Soldiers International :** Kitabu cha uhimizaji kuhusu kuzuia kutumiwa kwa watoto kama waaskari katika Jamhuri ya Kide-mokrasia ya Congo, 2018 : https://www.child-soldiers.org/shop/livret-de-sensibilisation-rdc. Kwa kukipata kitabu hiki, tuma simu kwa namba : + 243 813 182 039 ao +243991102747.
- **Msaada wa kiufundi kuhusu mazungumzo na makundi yenyi kumiliki silaha :** tuma simu kwa Shirika ama Geneva Call, namba +243 824 770 703 (katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo), ao +41 22 879 1050 (Uswisi).
- **Namba 117 : simu kwa ajili ya msaada kwa watoto katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.** Namba hii imetiwa kwa kuwasikiliza na kuwatolea mashauri watoto wenyi kuwa katika shida, na ku-wawezesha wakutane kwepesi na wote wanaoweza kuwasaidia. Vijana wanawake (na watu wote wanaotamani kuwasaidia) wanaweza kuitumia namba hii, iliyo bila malipo kwa Tigo, Orange, Voda-com na Airtel.

Kwa kupata kitabu hiki, tumia : info@child-soldiers.org

Yaliyomo



Child Soldiers International imeundwa mwaka 1998, na kazi yake ni kuzuia, duniani kote, kuorozeshwa kwa watoto katika kazi ya kiaskari, hata kwa njia gani. Kwa hiyo, tunajikaza kuheshimisha na kuimarisha sheria za nchi na za kimataifa, kutolea msaada wa kiufundi kwa serkali, kuleta msaada wa pesa na wa vitu kwa ofisi zenyi kuhusika na ukingo wa mtoto, na kusaidia jamii katika kazi ya kuzuia kuorozeshwa kwa watoto.

CHILD SOLDIERS INTERNATIONAL

Child Soldiers International
9 Marshalsea Road
London, SE1 1EP
+44 (0) 20 7367 4110
info@child-soldiers.org
www.child-soldiers.orgt